

MKATABA WA UPANGISHAJI GODOWN NA OFISI

KATI YA

**MICHAEL LAMECK NG'AHALA
(MWENYE NYUMBA)**

NA

**MALC INVESTMENT COMPANY LIMITED
(MPANGAJI)**

**KATIKA ENEO LENYE UKUBWA WA EKARI NNE (4) LILILOPO
KWENYE MKOA WA NJOMBE, WILAYA YA LUDEWA, KIWANJA
NAMBA 6 KITALU "17" MTA A WA MALANGALI**


A circular blue notary seal for Immanuel Bwire Musingi, an Advocate, Notary Public, and Commissioner for Oaths. The seal includes the text "Immanuel Bwire Musingi", "Bar 57 Dodoma", and "Advocate, Notary Public & Commissioner for Oaths". The seal also features a central emblem with a scale of justice and a book.

MKATABA WA KUPANGISHA GODOWN NA OFISI.

MKATABA huu umefanyika leo tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2025

KATI YA

MICHAEL LAMECK NG'AHALA mwenye simu no. **075690000** wa S.L.P 19 Njombe, kwa upande mmoja (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MWENYE NYUMBA"), NA

MALC INVESTMENT COMPANY LIMITED wa S.L.P 19 Njombe (ambaye katika mkataba huu ataitwa "MPANGAJI").

KWA KUWA mwenye eneo ni mmiliki halali wa eneo lililopo kiwanja Na. 6 Kitalu '17' MLANGALI katika Kata ya Mlingali ndani ya Mkoa wa Njombe; na

KWA KUWA mpangaji amemwendea mwenye eneo kwa nia ya kutaka kupangisha Godown na Ofisi kwa ajili ya shughuli za kiwanda cha kutengenezea plastiki (plastic) kwa muda wa kipindi cha miaka kumi (10) kwa malipo ya kodi iliyokubaliwa katika mkataba huu na kwa mujibu wa masharti mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu; na

KWA KUWA mwenye eneo amekubali kumpangisha mpangaji katika eneo hilo;

HIVYO BASI, MKATABA huu unashuhudia na kuthibitisha kama ifuatavyo:

1. **KWAMBA** Mwenye eneo amepangisha mpangaji eneo kwa ajili ya shughuli za kiwanda cha kutengenezea plastiki (plastic) katika eneo lililotajwa hapo juu kwa kiasi cha kodi ya Tshs. Milioni tano (Tshs. 5,000,000/-) tu, kwa mwezi bila ongezeko lolote na kwa muda wa miaka kumi (10) kwamba fedha hizo zitalipwa kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) hivyo itakua inalipwa kiasi cha shilingi milioni sitini (Tshs.60,000,000/-) tu kwa mwaka Na jumla ya kiasi cha shilingi milioni mia tano (500,000,000/=) kwa miaka kumi (10).
2. **KWAMBA** mpangaji atanza kupanga eneo hilo kuanzia tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2025 hadi tarehe 01 mwezi 08 mwaka 2035 ambapo mkataba huu utakoma.
3. **KWAMBA**, ikiwa Mpangaji anatimiza masharti yote ya ulipaji kodi na mengineyo, Mwenye eneo anampangisha mpangaji eneo hilo bila kumuingilia katika kipindi chote cha upangaji huo.



4. KWAMBA Mpangaji anatakiwa azingatie usafi wa eneo pamoja na mazingira yake na anatakiwa atumie eneo hilo kwa shughuli za kiwanda tu na sio vinginevyo
5. KWAMBA Mpangaji anatakiwa azingatie kulipa kodi kama inavyotakiwa na kuilipa kwa wakati kama ilivyokubaliwa katika mkataba huu.
6. KWAMBA Mwenye eneo, kwa wakati muafaka anayo haki ya kuingia katika eneo hilo pale inapobidi.
7. KWAMBA Mpangaji anatakiwa alipie ulinzi, maji na umeme katika eneo hilo kwa muda wote atakaopanga eneo hilo na wakati wa kuondoka katika eneo hilo atahakikisha kuwa hataacha madeni yoyote yanayohusiana na umeme na maji.
8. KWAMBA Mpangaji haruhisiwi kukodisha eneo hilo alilopanga kwa mtu mwingine yeyote bila ya idhini ya maandishi kutoka kwa Mwenye eneo, na ikiwa Mpangaji atashindwa kuendelea na Mkataba basi mpangaji atamrudishia mwenye eneo.
9. KWAMBA Mpangaji ahakikishe kwamba kwa wakati wote atakaokuwa kwenye eneo hilo hatawaghasi majirani wenzake kwa njia yoyote ile.
10. KWAMBA Mpangaji amjulishe mwenye nyumba kwa maandishi mwanzo wa miezi sita (6) wa mwisho wa mkataba huu endapo atapenda kuendelea na mkataba huu mara utakapokwisha.
11. KWAMBA Mpangaji na Mwenye eneo wanaweza kusitisha mkataba huu kwa kutoa taarifa kwa maandishi mwezi mmoja kabla.
12. KWAMBA Maneno "Mwenye eneo" na "Mpangaji" yatahusu familia, jamii na wategemea wa kila mmoja wao kwa madhumuni ya mkataba huu.

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa sahihi na Mwenye eneo na Mpangaji mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA
na **MICHAEL LAMECK NG'HALA**
leo hii
tarehe 01. mwezi 08. mwaka 2025

Handwritten signature

MMILIKI

MBELE YANGU:

SAINI

JINA: EMMANUEL BWIRE MUYENGI

SANDUKU LA POSTA: 57, DODOMA

WADHIFA: WAKILI



IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA
Na **MALC INVESTMENT COMPANY LIMITED**
leo hii
tarehe ... mwezi mwaka 2025



IMESAINIWA NA:
SAINI
JINA:
WADHIFA:

MBELE YANGU:
SAINI
JINA: EMMANUEL BWIRE MUYENGI
SANDUKU LA POSTA: 57, DODOMA
WADHIFA: WAKILI

